# KAMISHENI YA KUSIMAMIA NGUMI ZA KULIPWA

# TANZANIA PROFESSIONAL BOXING REGULATORY COMMISSION (TPBRC)

## KANUNI ZA MASHINDANO

SPORTS ASSOCIATION & CLUBS
Box 20116
25 MAR 2024
DAR ES SALAAM
NATIONAL SPORTS COUNCIL OF TANZANIA

## UTANGULIZI

Kanuni hizi zinahusisha sheria, taratibu na kanuni za uendeshaji wa mashindano ya mchezo wa ngumi za kulipwa zenye lengo pia la kulinda afya na maslahi ya bondia, maslahi ya waandaaji katika kuleta maendeleo na ukuzaji pamoja na kuuweka karibu mchezo wa ngumi za kulipwa kwa jamii. Hivyo basi, Kamisheni itazitumia Kanuni hizi katika kuendesha mashindano ya ngumi za kulipwa Tanzania.

## 1.0. SHERIA NA KANUNI ZA VYAMA VINAVYOENDESHA UBINGWA KIMATAIFA

Ili kutenda haki, kulinda afya, hadhi na maslahi miongoni mwa wadau wote wa ngumi za kulipwa, kwa mapambano ya ubingwa wa kimataifa, utekelezaji wa sheria na taratibu zote zitakazofuatwa ni za chama husika ambazo zitasomwa na kufafanuliwa kwa mabondia na maofisa wa mchezo husika katika kikao cha pamoja kati ya mabondia maofisa wa mchezo huo pamoja wawakilishi wa chama hicho na viongozi wa Kamisheni .

Katika Maktaba yake, Kamisheni itakuwa na nakala kamilifu ya Sheria na Kanuni za Vyama vya kimataifa vya masumbwi (championship sanctioning bodies) vinavyotambulika duniani.

## 2.0. BONDIA WA NGUMI ZA KULIPWA

Kulingana na sheria na taratibu za kimataifa za mtu kutambulika kama bondia wa kulipwa; mtu yeyote nchini Tanzania, atatambulika kama bondia wa kulipwa endapo atakuwa ametimiza vigezo na masharti yote yafuatayo: -

2.1. Awe ametimiza umri wa zaidi ya miaka kumi na nane (18) wakati anajiunga katika mchezo wa ngumi za kulipwa na atalazimika kuwa na leseni ya ngumi za kulipwa kabla hajaanza kupanda ulingoni. Ili kuthibitisha umri wake, bondia atawajibika kuwasilisha nakala halisi ya kitambulisho chochote kinachotolewa na serikali kama vile; kadi ya mpiga kura, leseni

REGISTRAR OF SPORTS ASSOCIATION & CLUBS
P. O. Box 20116
25 MAR 2024
DAR ES SALAAM
NATIONAL SPORTS COUNCIL OF TANZANIA

**UTANGULIZI**

Kanuni hizi zinahusisha sheria, taratibu na kanuni za uendeshaji wa mashindano ya mchezo wa ngumi za kulipwa zenye lengo pia la kulinda afya na maslahi ya bondia, maslahi ya waandaaji katika kuleta maendeleo na ukuzaji pamoja na kuuweka karibu mchezo wa ngumi za kulipwa kwa jamii. Hivyo basi, Kamisheni itazitumia Kanuni hizi katika kuendesha mashindano ya ngumi za kulipwa Tanzania.

**1.0. SHERIA NA KANUNI ZA VYAMA VINAVYOENDESHA UBINGWA KIMATAIFA**

Ili kutenda haki, kulinda afya, hadhi na maslahi miongoni mwa wadau wote wa ngumi za kulipwa, kwa mapambano ya ubingwa wa kimataifa, utekelezaji wa sheria na taratibu zote zitakazofuatwa ni za chama husika ambazo zitasomwa na kufafanuliwa kwa mabondia na maofisa wa mchezo husika katika kikao cha pamoja kati ya mabondia maofisa wa mchezo huo pamoja wawakilishi wa chama hicho na viongozi wa Kamisheni .

Katika Maktaba yake, Kamisheni itakuwa na nakala kamilifu ya Sheria na Kanuni za Vyama vya kimataifa vya masumbwi (championship sanctioning bodies) vinavyotambulika duniani.

**2.0. BONDIA WA NGUMI ZA KULIPWA**

Kulingana na sheria na taratibu za kimataifa za mtu kutambulika kama bondia wa kulipwa; mtu yeyote nchini Tanzania, atatambulika kama bondia wa kulipwa endapo atakuwa ametimiza vigezo na masharti yote yafuatayo: -

2.1. Awe ametimiza umri wa zaidi ya miaka kumi na nane (18) wakati anajiunga katika mchezo wa ngumi za kulipwa na atalazimika kuwa na leseni ya ngumi za kulipwa kabla hajaanza kupanda ulingoni. Ili kuthibitisha umri wake, bondia atawajibika kuwasilisha nakala halisi ya kitambulisho chochote kinachotolewa na serikali kama vile; kadi ya mpiga kura, leseni

REGISTRAR OF SPORTS ASSOCIATION & CLUBS
P. O. Box 20116
25 MAR 2024
DAR ES SALAAM
NATIONAL SPORTS COUNCIL OF TANZANIA

ya kuendesha vyombo vya moto, kitambulisho cha NIDA, hati ya kusafiria, n.k.

2.2. Ni muhimu awe amecheza mizunguko isiyopungua hamsini (50) kwenye ngumi za ridhaa.

2.3. Iwapo ataanzia moja kwa moja katika ngumi za kulipwa atalazimika kucheza mapambano ya mizunguko minne (4) yasiyopungua sita (6) yenye mizunguko isiyopungua ishirini na nne (24) na mapambano ya mizunguko sita (6) yasiyopungua manne (4) yenye jumla ya mizunguko ishirini na nne (24).

Kamati ya Ufundi ya Kamisheni inaweza kuruhusu bondia ambaye ataonesha umahiri na ustadi, kushiriki mapambano ya mizunguko zaidi kabla ya kukamilisha mizunguko iliyotajwa hapo endapo tu itajiridhisha na uwezo wa bondia huyo.

2.4. Bondia aliyecheza mizunguko kama ilivyoelekezwa katika aya ya 2.3. hapo juu anaruhusiwa kushiriki katika mapambano ya mtoano (elimination) ya kuwania ubingwa wa taifa,

REGISTRAR OF SPORTS ASSOCIATION & CLUBS
P. O. Box 20116
25 MAR 2024
DAR ES SALAAM
NATIONAL SPORTS COUNCIL OF TANZANIA

## 3.0. MADARAJA YA UZITO (WEIGHT DIVISIONS) YANAYOTAMBULIKA KATIKA MCHEZO WA NGUMI ZA KULIPWA.

### 3.1. Madaraja ya uzito

Uzito na madaraja ya uzito kwa mabondia wa kulipwa ambavyo vinatambulika katika Kamisheni ni viwango vya kimataifa vinavyokubaliwa na vyama vyote vya ngumi za kulipwa duniani. **NI LAZIMA** bondia afikie viwango vya uzito katika madaraja yaliyotajwa kama ilivyoorodheshwa katika jedwali la uzito hapa chini: -

| DARAJA | PAUNDI | USIOZIDI KILOGRAMU |
|---|---:|---:|
| Strawweight | 105 | 47.627 |
| Jr. Flyweight | 108 | 48.988 |
| Flyweight | 112 | 50.802 |
| Super Flyweight/ Jr. Bantamweight | 115 | 52.163 |
| Bantamweight | 118 | 53.525 |
| Super Bantamweight | 122 | 55.225 |
| Featherweight | 126 | 57.153 |
| Super Featherweight/Jr. Lightweight | 130 | 58.967 |
| Lightweight | 135 | 61.235 |
| Super Lightweight/Jr. Welterweight | 140 | 63.503 |
| Welterweight | 147 | 66.678 |
| Super Welterweight/Jr. Middleweight | 154 | 69.853 |
| Middleweight | 160 | 72.574 |
| Super Middleweight | 168 | 76.203 |
| Light Heavyweight | 175 | 79.378 |
| Cruiserweight | 190 | 86.183 |
| bridgerweight | 224 | 91 |
| Heavy Weight | 224+ | 101 |



REGISTRAR OF SPORTS ASSOCIATION & CLUBS
P. O. Box 20116
25 MAR 2024
DAR ES SALAAM
NATIONAL SPORTS COUNCIL OF TANZANIA

3.2. Bondio hatoruhusiwa kupigana endapo atazidi ukomo wa uzito kwa madaraja kama ifuatavyo: -

| Na. | Uzito (paundi) | Uzito (Kg) |
|---|---|---|
| | Uzito | |
| 1. | 118 | 53.552 |
| 2. | 118 – 130 | 53.552 – 58.995 |
| 3. | 130 – 140 | 58.995 – 63.531 |
| 4. | 140 – 175 | 63.531 – 79.407 |
| 5. | 175 – 190 | 79.407 – 86.211 |
| 6. | 190 – 200 | 86.211 – 90.747 |
| 7. | 200 – 224 | 91. 102 |
| 8. | 224+ | 102+ |

## 4.0. TARATIBU ZA UPIMAJI AFYA NA UZITO KWA MABONDIA NA MAOFISA

### 4.1. UPIMAJI AFYA

4.1.1. Kamisheni itaingia makubaliano na wadau wa afya kwa ajili ya kuendesha kitengo cha afya mahususi kwa ajili ya upimaji wa afya kwa mabondia na maofisa wa ulingoni na usimamizi wake katika mapambano ya ngumi za kulipwa.Muandaaji hatoruhusiwa kuingia makubaliano yoyote yanayohusiana na kitengo cha afya na hatowajibika kulipa gharama yoyote inayohusiana na upimaji wa afya pamoja na usimamizi wa afya katika pambano lake.

4.1.2. Siku 14 kabla ya kushiriki pambano lolote la ngumi za kulipwa bondia atawajibika kupimwa afya yake na daktari mwenye leseni ya Kamisheni na anayetambulika na chama cha madaktari wa tiba za michezo (TASMA). Kutokana na majibu ya vipimo, daktari atashauri iwapo bondia husika anaweza au hawezi kushiriki pambano.



REGISTRAR OF SPORTS ASSOCIATION & CLUBS
P. O. Box 20116
25 MAR 2024
DAR ES SALAAM
NATIONAL SPORTS COUNCIL OF TANZANIA

Daktari wa ulingoni atateuliwa na Kamisheni na atawasilisha taarifa yake masaa 48 tangu kumalizika kwa pambano.

4.1.3. Endapo bondia hatotokea kupima afya siku na mahali palipopangwa atapewa adhabu ya kulipa faini ya Shilingi laki mbili (200,000) pamoja na kupangiwa siku nyingine ya kupima afya.

4.1.4. Endapo bondia atagoma kupima afya atapewa adhabu ya kufungiwa kwa muda wa miezi 24.

4.1.5. Kamisheni itazingatia ushauri wa daktari kuhusu hali ya afya na uwezo wa bondia husika kiafya katika kushiriki pambano na **HAITARUHUSU** bondia kupigana iwapo daktari atashauri bondia husika asicheze katika pambano hilo kutokana na sababu za kiafya.

4.1.6. Bondia atakayeshindwa pambano kwa TKO au KO atasimamishwa kushiriki mapambano ya ngumi za kulipwa kwa kwa muda wa siku 21.

4.1.7. Bondia yeyote atakayefanya udanganyifu wa kupelekea kupoteza pambano ulingoni kwa pambano litakalofanyika Tanzania na udanganyifu huo kuthibitishwa na Kamisaa wa pambano hilo, atafungiwa kupigana ngumi kwa miezi ishirini na nne (24) na atakatwa asilimia hamsini (50%) ya malipo yake kwa mujibu wa mkataba.

4.1.8. Kila anapohuisha leseni yake, bondia au ofisa wa ulingoni atawajibika pia kupima afya chini ya usimamizi wa daktari mwenye leseni ya Kamisheni na kutiwa saini na daktari huyo kisha



REGISTRAR OF SPORTS ASSOCIATION & CLUBS
P. O. Box 20116
25 MAR 2024
DAR ES SALAAM
NATIONAL SPORTS COUNCIL OF TANZANIA

kuwasilisha matokeo ya vipimo vya afya yake kama itakavyoelekezwa na Kamisheni.

4.2. KUPIMA UZITO NA AFYA

4.2.1. Zoezi la kupima uzito litafanyika siku moja kabla ya pambano na litaanza saa tano kamili (05:00) asubuhi. Muandaaji atawajibika kuhakikisha eneo na miundo mbinu itakayotumika kupima uzito iko tayari saa moja kabla ya zoezi hilo kuanza. Muandaaji atapigwa faini ya Shilingi laki tano (500,000) kwa kuchelewesha kuanza kwa zoezi la kupima uzito kwa zaidi ya dakika 30.

4.2.2. Kamisheni itamteua msimamizi wa zoezi la kupima uzito. Msimamizi huyo atawajibika kuhakikisha kwamba: -

4.2.2.1. Ili kuakiki uzito wa mabondia itatumika mizani miwili kuthibitisha ulinganifu.

4.2.2.2. Amevaa sare iliyotolewa na Kamisheni wakati wote wa zoezi la kupima uzito likiendelea.

4.2.2.3. Taratibu nyingine zote zinafuatwa kwaa ukamilifu wake ikiwemo kutumia nyaraka rasmi zinazotolewa na Kamisheni kwa ajili ya kurekodi taarifa.

Msimamizi atapewa adhabu ya faini isiyopungua Shilingi Laki Mbili (200,000) endapo atakiuka kipengele chochote kati ya Ibara ya 4.2.

4.2.3. Mabondia, maofisa wa ulingoni pamoja na msimamizi wa zoezi la upimaji uzito watawajibika kuwepo katika eneo lililopangwa kwa zoezi la kupima uzito angalau saa moja kabla ya zoezi hilo



REGISTRAR OF SPORTS ASSOCIATION & CLUBS
P. O. Box 20116
25 MAR 2024
DAR ES SALAAM
NATIONAL SPORTS COUNCIL OF TANZANIA

kuanza. Adhabu ya kuchelewa kufika eneo la kupima uzito ni faini isiyopungua Shilingi Laki Mbili (200,000).

4.2.4. Mabondia wote wanaopigana, **WATALAZIMIKA: -**

4.2.4.1. kupima uzito ndani ya masaa ishirini na nne (24) au kumi na mbili (12) kabla ya pambano husika.

4.2.4.2. ni jukumu la Kamisheni kuleta mzani wa kupimia uzito kwa mabondia na itawajibika kuhakikisha mzani huo unakuwepo katika eneo lililopangwa kwa zoezi hilo angalau saa moja kabla zoezi la kupima uzito kuanza rasmi kwa muda uliopangwa ili kuwapa fursa mabondia kubaini uzito wao kabla ya kuanza rasmi kwa zoezi la upimaji uzito,

4.2.4.3. Kwa mapambano ya Kimataifa;

4.2.4.3.1. Bondia kutoka nje ya Tanzania atawajibika kuwasilisha kwa msimamizi wa zoezi la kupima uzito nakala halisi ya ruhusa ya kucheza nje ya nchi (clearence) iliyotolewa na mamlaka inayohusika na kusimamia ngumi za kulipwa nchini mwake kabla ya kuanza kwa zoezi la kupima uzito na afya.

4.2.4.3.2. Muandaaji atawajibika kuwasilisha nakala ya mkataba wa pambano kati yake na bondia kutoka nje ya Tanzania pamoja na taarifa ya matokeo ya vipimo vya afya kwa Kamisheni siku kumi (10)



REGISTRAR OF SPORTS ASSOCIATION & CLUBS
P. O. Box 20116
25 MAR 2024
DAR ES SALAAM
NATIONAL SPORTS COUNCIL OF TANZANIA

kabla ya pambano na atawasilisha nakala halisi za nyaraka hizo kabla ya zoezi la kupima uzito na afya halijafanyika.

4.2.5. Katika zoezi la upimaji uzito, mabondia watavaa nguo zenye kusitiri maungo yao na kuthibitishwa na msimamizi wa zoezi hilo kabla hawajapanda kwenye mzani.

4.2.6. Matokeo ya zoezi la upimaji uzito kwa mabondia ndiyo yatakayobainisha daraja la uzito kwa bondia husika na aidha kuendelea au kutoendelea kwa pambano pamoja na taratibu nyingine kama inavyobainishwa katika aya zinazofuata chini: -

4.2.6.1. Endapo bondia atakutwa na uzito zaidi ya anaopaswa kuwa nao kwa mujibu wa mkataba wa pambano wakati wa zoezi la upimaji uzito, atapewa muda wa masaa mawili (2) ili aweze kupunguza uzito huo na kufikia kiwango kinachostahili. Endapo bondia aliyezidi uzito atashindwa kupunguza uzito katika muda huo, hatoruhusiwa kucheza pambano husika.

4.2.6.2. Endapo, kwa sababu yoyote ile, zoezi la kupima uzito litafanyika masaa kumi na mbili kabla ya pambano, hakutakuwa na ruhusa ya kupunguza uzito na bondia aliyezidi uzito hatoruhusiwa kupigana.

4.2.6.3. Endapo mabondia watapima uzito kwa ajili ya pambano la ubingwa wa taifa; na bingwa anayetetea ubingwa atakutwa na uzito zaidi ya kiwango anachotakiwa kuwa nacho na akashindwa

REGISTRAR OF SPORTS ASSOCIATIONS & CLUBS
P. O. Box 20116
25 MAR 2024
DAR ES SALAAM
NATIONAL SPORTS COUNCIL OF TANZANIA

kuupunguza uzito huo katika muda wa ziada kama ilivyoelekezwa hapo juu, basi bingwa huyo atapoteza ubingwa wake papo hapo kwa mtindo unaojulikana kama "*kupoteza ubingwa kwenye mizani*".

4.2.6.4. Bila ya kuathiri maelekezo ya hapo juu, pambano litaendelea kuwa la ubingwa kwa upande wa mpinzani endapo mpinzani huyo atafikisha uzito uliohitajika kwa pambano husika,

4.2.6.5. Endapo mpinzani atazidi uzito na bingwa atafikisha uzito; na bingwa akashinda pambano hilo, ubingwa bado utaendelea kushikiliwa na bingwa,

4.2.6.6. Endapo mpinzani atazidi uzito na kushinda pambano hilo, Kamisheni itautangaza ubingwa huo kuwa wazi.

4.2.6.7. Endapo mabondia wote hawatafikisha kabisa uzito unaostahili kwa ajili ya pambano husika, pambano hili linaweza kuendelea kufanyika likiwa pambano lisilo la ubingwa (non title fight) na ubingwa husika utakuwa wazi,

4.2.6.8. Endapo pambano litahairishwa kwa muda unaozidi masaa ishirini na nne (24), mabondia watalazimika kupima tena uzito.

4.2.6.9. Mara baada ya zoezi la kupima uzito na afya kukamilika, msimamizi wa zoezi la kupima uzito na afya, mabondia pamoja na timu zao watafanya kikao



REGISTRAR OF SPORTS ASSOCIATION & CLUBS
P. O. Box 20116
25 MAR 2024
DAR ES SALAAM
NATIONAL SPORTS COUNCIL OF TANZANIA

(rules meeting) ambapo pamoja na mambo mengine: -

i) Msimamizi atawakumbusha juu ya sheria na kanuni za ulingoni,

ii) Mabondia wataorodhesha majina ya wasaidizi wao wa ulingoni. iii) Mabondia watachagua na kukubaliana juu ya kona zao ulingoni,

5.0. **KANUNI NA TARATIBU ZA MAPAMBANO YA UBINGWA WA TAIFA NA KIMATAIFA,**

Mapambano yote ya ubingwa wa Taifa na kimataifa yanayofanyika Tanzania kati ya mabondia wa Tanzania na au bondia wa nje ya Tanzania yatafanyika kwa kufuata utaratibu ufuatao:-

5.1. Ubingwa wa taifa

Kamisheni ndio itakua na wajibu wa kuidhinisha kufanyika kwa mapambano ya ubingwa wa Taifa baada ya wakuzaji kuwasilisha maombi ya kuandaa mapambano ya ubingwa wa taifa.

5.2. Kamisheni itaendesha mapambano ya ubingwa wa taifa kwa nafasi za ubingwa zilizo wazi ili kutoa fursa kwa mabondia waliokidhi vigezo kushindania ubingwa wa taifa ikiwemo kuwa katika orodha ya mabondia 20 bora katika kanzidata ya Boxrec (www.boxrec.com) katika uzito wake,

5.3. Bingwa wa Tanzania atalazimika kutetea ubingwa wake kwa hiyari katika kipindi cha miezi sita (6) tangu alipotwaa ubingwa huo kwa kupambana na mmoja kati ya mabondia wanaotambuliwa katika orodha ya mabondia ishinirini (20) bora wa uzito wake.



REGISTRAR OF SPORTS ASSOCIATION & CLUBS
P. O. Box 20116
25 MAR 2024
DAR ES SALAAM
NATIONAL SPORTS COUNCIL OF TANZANIA

5.4. Endapo bingwa atashindwa kuutetea ubingwa wake baada ya kupita miezi sita (6) Kamisheni itautangaza ubingwa huo kuwa wazi,

5.5. Bila ya kuathiri aya 5.3. hapo juu, ubingwa utakuwa wazi ikiwa mambo yafuatayo yatatokea kwa pamoja au moja kati ya hayo kwa bondia anayeshikilia ubingwa: -

5.5.1. Atapewa adhabu na Kamisheni kutokana na makosa ya utovu wa nidhamu au makosa mengine ambapo adhabu yake itakuwa ya kufungiwa kwa zaidi ya miezi kumi na mbili (12),

5.5.2. Atasimamishwa kupigana kutokana na sababu za kiafya,

5.5.3. Atapoteza ubingwa endapo atashindwa pambano la uzito ambao yeye ni bingwa.

5.5.4. Atathibitika kutumia madawa na mbinu haramu michezoni,

5.6. Mapambano ya kimataifa

Katika kukuza mchezo na viwango vya ushindani kwa mabondia, Kamisheni inaweza kutoa idhini kwa mapambano ysiyo ya ubingwa na ya ubingwa wa kimataifa kwa vyama vinavyotambuliwa kuendesha mapambano ya ubingwa wa kimataifa kulingana na vigezo vifuatavyo: -

5.6.1. Kamisheni pekee ndio itakua na wajibu wa kuidhinisha kufanyika kwa mapambano yasiyo ya ubingwa na ya ubingwa wa kimataifa yanayofanyika Tanzania baada ya muandaaji kukamilisha taratibu zote za msingi zinazohusiana na pambano la kimataifa kama vile: -

5.6.1.1. Kuthibitisha mkataba kati ya muandaaji na bondia angalau siku kumi (10) kabla ya pambano,



REGISTRAR OF SPORTS ASSOCIATION & CLUBS
P. O. Box 20116
25 MAR 2024
DAR ES SALAAM
NATIONAL SPORTS COUNCIL OF TANZANIA

5.6.1.2. Kuwasilisha ruhusa ya kucheza nchini toka katika chombo cha kusimamia ngumi za kulipwa katika nchi anayotokea ikiwemo Zanzibar siku kumi (10) kabla ya pambano. Ikiwa bondia kutoka nje ya Tanzania hatowasilisha ruhusa ya kucheza kutoka katika nchi ambayo ni raia au mkazi wake, atawajibika kukata leseni ya Kamisheni kwa ajili ya pambano hilo tu mara baada ya uthibitishwa utimamu wa afya yake na daktari.

5.6.1.3. Kuwasilisha taarifa ya afya ya bondia kwa Kamisheni siku kumi (10) kabla ya pambano,

5.6.1.4. Kuwasilisha kibali cha kuendesha pambano la ubingwa kimataifa kutoka chombo husika (sanctioning organization)kinachoendesha ubingwa huo siku kumi (10) kabla pambano,

5.6.1.5. Muandaaji hataruhusiwa kuwa na ubingwa (mkanda) wake

5.7. Mapambano yote hayatazidi mizunguko kumi na mbili (12 rounds) kwa wanaume na mizunguko kumi (10) kwa wanawake; hayatapungua mizunguko minne (4 rounds) yenye dakika tatu (3) kwa wanaume na dakika mbili (2) kwa wanawake kwa mzunguko mmoja na mapumziko ya dakika moja (1) kati ya mzunguko mmoja na mzunguko unaofuata,

5.8. Mikataba ya kushiriki mapambano ya ngumi za kulipwa kwa mabondia.

5.8.1. Mikataba yote ya ngumi za kulipwa kati ya bondia na muandaaji kwa ajili ya kushiriki pambano itatolewa na Kamisheni itazingatia Sheria ya Mikataba, Sura ya 345 ya Sheria za Tanzania pamoja vipengele vyote muhimu vya



REGISTRAR OF SPORTS ASSOCIATION & CLUBS
P. O. Box 20116
25 MAR 2024
DAR ES SALAAM
NATIONAL SPORTS COUNCIL OF TANZANIA

uandaaji wa mikataba ya mapambano ya ngumi za kulipwa ikiwemo: -

5.8.1.1. Kutaja waziwazi; jina la bondia anayesaini mkataba,

5.8.1.2. Jina la bondia atakayepambana naye,

5.8.1.3. Uzito watakaopigania,

5.8.1.4. Tarehe na mahali pambano litakapofanyika,

5.8.1.5. Malipo ya bondia (purse fee) kwa kushiriki pambano hilo.

5.8.1.6. Kwa pambano litakalofanyika ndani ya nchi, bondia kutoka nje ya Tanzania atakatwa asilimia 3 (%) ya malipo ya mkataba wa pambano na fedha hizo zitaingizwa kwenye akaunti ya benki ya Kamisheni.

REGISTRAR OF SPORTS ASSOCIATION & CLUBS
P. O. Box 20116
25 MAR 2024
DAR ES SALAAM
NATIONAL SPORTS COUNCIL OF TANZANIA

## 6.0. KANUNI NA SHERIA ZA ULINGONI

6.1. Kamisheni ya Kusimamia Ngumi za Kulipwa Tanzania inatumia Sheria Jumuishi (Unified Rules) ambazo huandaliwa na "Association of Boxing Commissions" za mwaka 2001 pamoja na marekebisho yake ambayo hufanyika mara kwa mara kwa mapambano yasiyo ya ubingwa. Nakala ya Sheria hizo itaambatishwa pamoja na Kanuni hizi. Wakati wote nakala ya Kingereza ndiyo itakayotumika kutoa tafsiri rasmi. Kamisheni itaanda nyaraka ya lugha ya kiswahili ya tafsiri ya Kanuni hizo kwa ajili ya matumizi kujifunzia tu.

6.2. Kwa mapambano ya ubingwa wa Kimataifa, zitatumika sheria na kanuni za vyama husika ambazo zitathibitishwa na Kamisheni kabla ya kutumika kwake.

6.3. Kamisaa/Kamishna (supervisor) wa pambano atawajibika kuwasilisha taarifa ya pambano kwa maandishi ndani ya masaa 24 tangu kumalizika kwa pambano husika na kwa mapambano ya ubingwa wa kimataifa kamisaa (supervisor) wa pambano hilo atawajibika kuwasilisha nakala ya taarifa ya pambano hilo kwa Kamisheni ndani yaa masaa 48 tangu kukamilika kwa pambano husika. Kamisaa atakaposhindwa kuwasilisha taarifa kwa wakati ataondolewa kwenye orodha ya makamisaa.

## 7.0. WATOA HUDUMA KATIKA MCHEZO WA NGUMI ZA KULIPWA PAMOJA NA MAJUKUMU YAO

Kamisheni inatambua kwamba, watoa huduma ni kada muhimu katika kuendeleza mchezo wa ngumi za kulipwa Tanzania. Watoa huduma wanawajibika kwanza kuwa wanachama katika vyama shiriki kwenye kada husika ili waweze kupatiwa huduma kulingana na leseni inayotolewa na Kamisheni. Mwisho wa matumizi ya leseni ni kila ifikapo tarehe 31 Juni . Watoa



REGISTRAR OF SPORTS ASSOCIATION & CLUBS
P. O. Box 20116
25 MAR 2024
DAR ES SALAAM
NATIONAL SPORTS COUNCIL OF TANZANIA

huduma hao ni; mkufunzi (coach/trainer), Msimamizi (Manager), msaidizi wa bondia ulingoni (second, corner man, cutman), Muandaaji/mkuzaji (promoter), matchmaker, daktari, "ring announcer", n.k. ofisa wa ulingoni (mtunza muda/mwamuzi/jaji/mkaguzi/msimamizi), "card girl", n.k. na majukumu yao yameorodheshwa hapa chini kama ifuatavyo: -

7.1. Mkufunzi/kocha (trainer/coach)

Atakuwa ni mtu mwenye taaluma/uzoefu wa kutoa mafunzo ya mchezo wa ngumi za kulipwa ambaye atakuwa na jukumu la kumfundisha bondia mbinu na stadi za kupigana katika mapambano ya ngumi za kulipwa pamoja na sheria za ulingoni. Mkufunzi atakuwa mwanachama wa chama makocha.

7.2. Msimamizi/Meneja (manager)

Meneja ni mtu binafsi au kampuni (kwa tafsiri ya sheria za makampuni na majina ya biashara za Tanzania) ambayo bondia ameingia nayo makubaliano ya kisheria ya kuwa wakala/mwakilishi wake mwenye majukumu ya kusimamia maslahi na masuala yote yanayohusiana na ukuzaji na uendelezaji wa kipaji chake pamoja na matumizi ya jina lake kama bidhaa ya kibiashara (brand). Mikataba kati ya meneja na bondia itasajiliwa pia katika Kamisheni,

7.3. Msaidizi wa bondia ulingoni ("second", corner man/cut man)

Msaidizi wa ulingoni ni msaidizi wa bondia anapokuwa ulingoni ambaye atakuwa na jukumu la kutoa huduma kwa bondia wakati wa mapambano. Msaidizi wa bondia ulingoni atakuwa mwanachama wa chama cha makocha

7.4. Mkuzaji/Muandaaji (promoter)



REGISTRAR OF SPORTS ASSOCIATION & CLUBS
P. O. Box 20116
25 MAR 2024
DAR ES SALAAM
NATIONAL SPORTS COUNCIL OF TANZANIA

Ni kampuni au jina la biashara ambalo limesajiliwa kwa mujibu wa Sheria ya Makampuni, Sura ya 212 na Sheria ya Usajili wa Majina ya Biashara, Sura ya 213 ya Sheria za Tanzania ambayo moja ya kazi zake ni kuwa Muandaaji wa michezo kama anavyotambulika kwa mujibu wa Kifungu cha 19 cha Kanuni za Usajili za Baraza la Michezo la Taifa za Mwaka 1999 na pia mwenye leseni ya Kamisheni. Wajibu wa Muandaaji ni kuandaa mapambano ya ngumi za kulipwa kwa: -

7.4.1. Kuingia makubaliano kati yake na mabondia pamoja na kulipa ada (purse money) ya wachezaji

7.4.2. Kulipa ada ya kibali (sanctioning fee) kwa Kamisheni moja kwa moja kwa mapambano ya kitaifa na kimataifa. Viwango vya malipo ya vibali ni kama ifuatavyo: -

7.4.3. Pambano kubwa; Shilingi Milioni Tano (5,000,000),

7.4.4. Pambano la kati; Shilingi Milioni Moja (1,000,000),

7.4.5. Pambano dogo; Shilingi Elfu Hamsini (50,000),

7.4.6. Pambano la wazi (exhibition) ambalo halitakuwa na kiingilio; bure

7.4.7. Kulipa ada ya maofisa wa ulingoni kwa Kamisheni moja kwa moja kwa mapambano ya kitaifa na kimataifa. Viwango vya malipo ya malipo hayo ni kama ifuatavyo: -

7.4.8. Pambano kubwa; Shilingi Milioni Nne na Laki Tano (4,500,000). Kila afisa wa ulingoni atalipwa kiasi cha Shilingi Laki Tano (500,000). Pambano kubwa litahudumiwa na maafisa wa ulingoni jumla 9



REGISTRAR OF SPORTS ASSOCIATION & CLUBS
P. O. Box 20116
25 MAR 2024
DAR ES SALAAM
NATIONAL SPORTS COUNCIL OF TANZANIA

7.4.9. Pambano la kati; Shilingi Milioni Mbili na Laki Nne (2,400,000). Kila afisa wa ulingoni atalipwa Shilingi Laki Tatu (300,000). Pambano la kati litahudumiwa na maafisa wa ulingoni jumla 9.

7.4.10. Pambano dogo; Shilingi Laki Tatu (300,000). Kila afisa wa ulingoni atalipwa Shilingi Elfu Hamsini.

7.4.11. Pambano la wazi (exhibition); Shilingi Laki Tatu (300,000). Kila afisa wa ulingoni atalipwa Shilingi Elfu Hamsini.

7.4.12. Kulipa ada ya kibali cha pambano katika Baraza la Michezo la Taifa.

7.4.13. Kiasi cha asilimia kumi (10) ya ada ya kibali cha pambano (sanctioning fees) kwa mapambano makubwa, kitatolewa na kugawanywa kwenye vyama shiriki.

Muandaaji/mkuzaji atakuwa mwanachama wa chama cha wakuzaji na mawakala.

7.5. Match Maker/wakala

Kwenye ngumi za kulipwa, "Matchmaker" ni mtu mwenye jukumu la kuwatafuta mabondia wenye vigezo kwa ajili ya kushiriki pambano husika kwa niaba ya muandaaji. Kwa mapambano ya Kimataifa, matchmaker/wakala atalipa asilimia moja (1%) malipo yake toka kwa bondia. Matchmaker/wakala atakuwa mwanachama wa chama cha wakuzaji/mawakala.



REGISTRAR OF SPORTS ASSOCIATION & CLUBS
P. O. Box 20116
25 MAR 2024
DAR ES SALAAM
NATIONAL SPORTS COUNCIL OF TANZANIA

7.6. Daktari (ring physician),

Mtu yeyote mwenye taaluma ya udaktari wa binadamu (doctor of medicine) na mwenye leseni ya kufanya kazi ya udaktari nchini Tanzania. Vilevile, kwa madhumuni ya Kanuni hizi, daktari pia anapaswa kuwa na ujuzi wa taaluma ya udaktari wa michezo (sports medicine) na mwanachama hai wa Chama cha Madaktari wa Tiba ya Michezo Tanzania (TASMA).

7.7. Mtunza muda (time keeper)

Ni mtu mwenye jukumu la kutunza muda wa pambano kwa kuhakikisha kila mzunguko unachezwa kwa muda uliopangwa na atagonga kengele kuashiria kuanza au kumalizika kwa mzunguko.

7.8. MC/Mtangazaji (Ring announcer)

Ni mtu ambaye atakuwa na jukumu la kutangaza matukio mbalimbali katika ukumbi panapofanyika mapambano ya ngumi za kulipwa.

7.9. Card girl

Ni mwanamke/msichana ambaye atakuwa na jukumu la kuonesha mzunguko unaofuata akiwa ulingoni.

7.10. Mkaguzi (inspector) na Msimamizi/Kamishna wa pambano (supervisor)

7.10.1. Mkaguzi

Mkaguzi ni mwanachama wa chama cha waamuzi wa ngumi za kulipwa na ambaye ana leseni amilifu na mwenye sifa na weledi wa utaratibu na kanuni za kumuandaa bondia ili aweze kupanda ulingoni. Mkaguzi atateuliwa na Kamisheni kuhakikisha mabondia wanakuwa na vifaa vinavyotakiwa na kuvitumia kwa usahihi kwa ajili ya bondia ikiwemo bandeji za kufunga mkononi kabla ya kuvaa glovu za kupigania, kiknga



REGISTRAR OF SPORTS ASSOCIATION & CLUBS
P. O. Box 20116
25 MAR 2024
DAR ES SALAAM
NATIONAL SPORTS COUNCIL OF TANZANIA

kinywa, kikinga korodani, mavazi sahihi kwa bondia na wasaidizi wake wa ulingoni na kadhalika.

7.10.2. Msimamizi wa pambano

Msimamizi wa pambano ni hatateuliwa na kamisheni ya ngumi za kulipwa kuhakikisha kila kitu kinachohusiana na pambano husika kwa upande wa utekelezaji wa majukumu ya waamuzi wa ulingoni, mabondia na wasaidizi wa ulingoni yanafanyika kwa usahihi, kwa wakati na kwa weledi.

**8.0. Utaratibu wa kuandaa mapambano ya ngumi za kulipwa Tanzania**

Kwa madhumuni ya Kanuni hizi, mapambano yote ya ngumi za kulipwa yatafanyika mara tu baada ya kupata idhini (sanction) ya Kamisheni. Utaratibu utakaofuatwa na waandaaji wa mapambano hayo ili kupata idhini ni kama ufuatao: -

8.1. Kuwasilisha maombi ya kuandaa pambano la ngumi za kulipwa

8.1.1. Mkuzaji atawasilisha taarifa ya nia ya kuandaa pambano la ngumi za kulipwa kwa chama cha Wakuzaji na Mawakala wa Ngumi za Kulipwa Tanzania. Nakala ya taarifa hiyo itatumwa kwa Kamisheni,

8.1.2. Siku tatu (3) baada ya kutoa taarifa hiyo, mkuzaji atawasilisha maombi ya kibali cha kuandaa pambano hilo katika Kamisheni kwa maandishi katika kipindi kisichopungua siku thelathini (30) kabla ya pambano. Nakala ya maombi yake itatumwa kwa Chama cha Wakuzaji na Mawakala wa Ngumi za Kulipwa na Chama cha Mabondia wa Ngumi za Kulipwa na atabainisha yafuatayo: -

8.1.2.1. Kampuni/jina la biashara la Muandaaji akiambatisha na nakala ya leseni yake iliyotolewa na Kamisheni,



REGISTRAR OF SPORTS ASSOCIATION & CLUBS
P. O. Box 20116
25 MAR 2024
DAR ES SALAAM
NATIONAL SPORTS COUNCIL OF TANZANIA

8.1.2.2. Nakala ya malipo ya ada ya mwaka ya Baraza la Michezo la Taifa.

8.1.2.3. Tarehe na mahali patakapofanyika pambano hilo,

8.1.2.4. Orodha ya mabondia watakaocheza katika pambano hilo akiambatisha na mikataba yao,

Mara baada ya maombi hayo kuthibitishwa, muandaaji atapaswa kutekeleza yafuatayo: -

8.1.3. Kulipia kibali cha kuandaa pambano husika (sanctioning fee) kwa Kamisheni na kuwasilisha hati ya malipo ya benki (bank pay-in slip) siku tatu (3) tangu kuthibitishwa,

8.1.4. Kuweka katika akaunti ya benki ya Kamisheni malipo yote ya mabondia kwa mujibu wa mikataba, malipo ya maofisa wa ulingoni na watoa huduma wengine watakaobainishwa kati yao na Muandaaji na kuwasilisha hati ya benki kwa ajili ya malipo hayo (bank pay-in slip) katika kipindi cha siku thelasini (30) kabla ya pambano.

8.1.5. Muandaaji ataweka nembo (logo) ya Kamisheni katika matangazo yote ya pambano lake ikiwemo mabango, n.k.

8.1.6. Muandaaji atatoa tiketi za hadhi ya VVIP zisizopungua 10 kwa Kamisheni.

REGISTRAR OF SPORTS ASSOCIATION & CLUBS
P. O. Box 20116
25 MAR 2024
DAR ES SALAAM
NATIONAL SPORTS COUNCIL OF TANZANIA

Kamisheni itaitisha mkutano na waandishi wa habari ili kuuarifu umma juu ya uwepo wa pambano husika au kutoidhinisha pambano husika siku saba (7) kabla ya pambano.

Kamisheni itatoa adhabu ya faini ya Shilingi za Kitanzania Milioni Moja (1,000,000) au kufungia leseni yake kwa muda wa mwaka mmoja au vyote kwa pamoja endapo Muandaaji atakiuka kipengele kimojawapo cha Ibara ya 8.

## 9.0. HAKI ZA MATANGAZO YA TELEVISHENI KWA MAPAMBANO YA NGUMI ZA KULIPWA.

Kamisheni inaweka utaratibu wa usimamizi na mgawanyo wa haki za matangazo na maudhui kama ifuatavyo:

9.1. Haki ya Maudhui

Mkuzaji ana haki ya kukubaliana na mtu, kampuni au taasisi yeyote kwa ajili ya kumuuzia maudhui (content) ya kwenye pambano lake.

9.2. Haki ya matangazo

Kamisheni itadhibiti haki ya matangazo kwa mapambano yote ya ngumi za kulipwa.

9.3. Mgawanyo wa haki za matangazo

Baada ya makato ya kodi, n.k. kiasi cha asilimia ishilini (20) ya mapato yatokanayo na fedha za uuzaji wa haki za matangazo zitagawiwa sawa kwa vyama shiriki na Kamisheni itabaki na asilimia themanini (80).

9.4. Kamisheni itatumia kona mbili kati ya nne za ulingo kwa kuweka nembo yake au ya wadhamini wake na maeneo mengine yaliyoobaki yatatumika na muandaaji kwa kadri atakavyoona inafaa.

## 10.0. UTARATIBU WA ULINGONI

REGISTRAR OF SPORTS ASSOCIATION & CLUBS
P. O. Box 20116
25 MAR 2024
DAR ES SALAAM
NATIONAL SPORTS COUNCIL OF TANZANIA

Siku ya pambano muandaaji atawajibika kuweka mazingira rafiki kwa mabondia wanaopambana kuweza kufanya maandalizi ya mwisho kabla ya kupanda na baada ya kushuka ulingoni kwa kufanya yafuatayo: -

10.1. Bondia atafika katika ukumbi wa kupigania masaa mawili kabla ya muda wa kuanza kwa mapambano na msimamizi wa pambano atawatambua bondia na timu yake ya wasaidizi wa ulingoni.

Bondia atakayefika nje ya muda wa masaa mawili kabla ya muda wa kuanza pambano ataadhibiwa kwa kupigwa faini isiyopungua Shilingi laki moja (100,000).

10.2. Mabondia watakaocheza kutokea kona ya nyekundu (red corner) watakaa tofauti na wenzao wa kona ya bluu (blue corner),

10.3. Bondia atapanda ulingoni kupigana akiwa peke yake na atakuwa na wasaidizi (seconds) wasiopunguna wawili (2) na wasiozidi wanne (4) kwa mapambano ya ubingwa na wasiozidi wawili (2) kwa mapambano yasiyo ya ubingwa ambao miongoni mwao ni lazima awepo kocha wake au cutman. Bondia na timu yake wataadhibiwa faini isiyopungua Shilingi laki mbili (200,000) ikiwa atakiuka kipengele hiki.

10.4. Katika mapambano yote bondia ataruhusiwa kuhudumiwa na msaidizi mmoja tu ndani ya ulingo wakati wa mapumziko ya dakika moja kati ya mzunguko na mzunguko. Kambi ya bondia itaadhibiwa faini isiyoungua laki mbili (200,000) ikiwa atakiuka kipengele hiki.

10.5. Bondia atamteua na kumtambulisha kwa mwamuzi mmoja kati ya wasaidizi wake wa ulingoni kuwa "chief second" katika pambano husika kwa maamuzi ya kisheria ulingoni,

REGISTRAR OF SPORTS ASSOCIATIONS & CLUBS
P. O. Box 20116
25 MAR 2024
DAR ES SALAAM
NATIONAL SPORTS COUNCIL OF TANZANIA

10.6. Wasaidizi wote wa ulingoni watapaswa kuwa na leseni kamilifu inayotolewa na Kamisheni wakati wakitimiza wajibu ulingoni,

10.7. Mashabiki wa bondia hawataruhusiwa kuingia ulingoni au kuwa kwenye kona ya mpinzani wakati pambano likiendelea. Bondia atapewa adhabu ya kupigwa faini isiyopungua Shilingi milioni moja (1,000,000).

10.8. Wasaidizi wa bondia wataruhusiwa kuwa na vifaa na dawa zilizoruhusiwa kwa matumizi ya bondia wakati akiwa ulingoni baada ya vifaa na dawa hizo kukaguliwa na kuthibitishwa na mkaguzi (inspector) wa mchezo husika.

10.9. Mwamuzi ndio atakuwa na maamuzi ya mwisho (sole arbitor) katika pambano husika ulingoni. Sheria hii haitazuia ukaguzi wa video au ukaguzi mwingine wa uamuzi uliofanywa na mwamuzi ulingoni chini ya taratibu za mamlaka ya udhibiti inayotumika ikiwa malalamiko yatawasilishwa kwa madai ya ukiukaji wa wazi wa kanuni.

10.10. Ikiwa bondia au timu yake wana malalamiko yoyote yatokanayo na pambano husika watawajibika kuyawasilisha malalamiko hayo katika Kamisheni kwa maandishi ndani ya masaa 24 tangu kumalizika kwa pambano akiambatisha vielelezo vyote. Bondia au timu yake wataadhibiwa kwa kufungiwa mwaka mmoja au faini isiyozidi Shilingi Laki Tano au vyote viwili ikiwa watashutumu waamuzi au Kamisheni akiwa juu au chini ya ulingo.

10.11. Maafisa wa ulingoni hawataruhusiwa kutoa maoni yao kwenye vyombo vya habari kuhusu uamuzi katika mapambano ya ngumi za kulipwa kabla au baada ya mapambano. Afisa atakayekiuka kipengele hiki

REGISTRAR OF SPORTS ASSOCIATIONS & CLUBS
P. O. Box 20116
25 MAR 2024
DAR ES SALAAM
NATIONAL SPORTS COUNCIL OF TANZANIA

ataadhibiwa faini isiyopungua Shilingi laki mbili (200,000) au kufungiwa kwa muda usiozidi mwaka mmoja au adhabu zote 2 kwa pamoja.

10.12. Endapo afisa yeyote wa ulingoni akiwa katika kutimiza majukumu yake ataharibu pambano kwa makusudi atachukuliwa hatua za kinidhamu ikiwemo kufungiwa kwa muda wa miezi 6 au kupigwa faini isiyopungua shilingi laki mbili (200,000) au vyote viwili kwa pamoja,

10.13. Muandaaji atawajibika kuweka uzio/kizuizi (barricade/barrier) kati ya majaji na mashabiki ili kuwapa fursa majaji kutimiza majukumu yao bila ya kubughudhiwa na mashabiki. Mapambano haya taanza mpaka takwa hili la Kikanuni litimizwe na muandaaji atapigwa faini ya shilingi 300,000 kwa kuchelewesha kuanza kwa mapambano kwa sababu ya kuchelewa kuweka uzio.

## 11.0. UTARATIBU WA KUSAFIRI NJE YA NCHI KWA AJILI YA MAPAMBANO YA NGUMI ZA KULIPWA

Panapotoke fursa kwa bondia kupata nafasi ya kwenda kupigana nje ya Tanzania; wakala/kocha/Msimamizi/ wa bondia atawajibika kuomba kibali kutoka Kamisheni kutoa taarifa ya pambano hilo katika chama cha wakuzaji/mawakala na chama cha mabondia. Katika maombi yake kwa Kamisheni, ataambatisha nyaraka zifuatazo: -

11.1. Mkataba wa pambano husika pamoja na barua za mwaliko,

11.2. Nakala ya hati za kusafiria kwa wote watakaoambatana na bondia katika safari hiyo,

11.3. Kabla ya Kamisheni kuwasilisha maombi ya Kibali cha kusafiri nje ya nchi katika Baraza la Michezo la Taifa kama kinavyoelekeza Kifungu cha 17 (1) na (4) cha Kanuni za Baraza la Michezo la Taifa za Mwaka



REGISTRAR OF SPORTS ASSOCIATIONS & CLUBS
P. O. Box 20116
25 MAR 2024
DAR ES SALAAM
NATIONAL SPORTS COUNCIL OF TANZANIA

1999, mwombaji atawajibika kulipa katika akaunti ya benki ya Kamisheni Shilingi Laki Moja (100,000) kwa kila bondia mmoja ikiwa ni ada ya kibali hicho kabla ya kusafiri.

11.4. Kamisheni itaandika barua ya kumruhusu bondia (clearence letter) kwa chombo cha kusimamia ngumi za kulipwa katika nchi ambayo bondia atakwenda kupigana,

11.5. Mara baada ya kurejea toka katika mashindano, wakala au bondia atawasilisha katika Kamisheni taarifa ya pambano aliloshiriki kwa maandishi ndani ya masaa 48 tangu arejee nchini. Adhabu ya kukiuka kipengele hiki ni faini isiyopungua shilingi laki tano (500,000) au kufungiwa mwaka mmoja au vyote viwili kwa pamoja.

## 12. MAREKEBISHO YA KANUNI

Kanuni hii inaweza kufanyiwa marekebisho wakati wowote endapo itahitajika kufanya hivyo kupitia Mkutano Mkuu wa wanachama. Marekebisho hayo yatahusisha kuongeza kifungu au vifungu, kubadili sentensi au maneno katika sentensi au kufuta kifungu au vifungu.

## 13. USAJILI WA KANUNI

Kanuni hizi zimepitishwa katika Mkutano Mkuu uliofanyika tarehe 09 mwezi 03, mwaka 2024, na kusasajiliwa kwa mujibu wa Sheria ya Baraza la Michezo la Taifa.

Jina na saini
CHAUREMBO PALASA
[signature]
Rais

Jina na saini
GEORGE SIWASI
[signature]
Katibu

REGISTRAR OF SPORTS ASSOCIATIONS & CLUBS
P. O. Box 20116
25 MAR 2024
DAR ES SALAAM
NATIONAL SPORTS COUNCIL OF TANZANIA